BODI YA MFUKO WA BARABARA



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TAARIFA FUPI KUHUSU BODI YA MFUKO WA BARABARA

Friday, 26 September 2008

TAARIFA FUPI KUHUSU BODI YA MFUKO WA BARABARA

1.0 UTANGULIZI

Kuundwa kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kugharimia matengenezo ya barabara, wakala wa Barabara wa Taifa, kusimamia mtandao wa barabara ni sehemu ya mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya barabara.

Inategemeawa kwamba mabadiliko yanayofanyika yatasaidia kupunguza kwa kiwango kikubwa, matatizo ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara, taratibu za utawala na uteuzi wa makandarasi na wahandisi washauri zinazochosha, wafanyakazi wasiopewa motisha wa kutosha ambavyo hapo zamani zilisababisha ucheleweshaji mkubwa wa miradi, kuzidi kwa gharama, mzigo mkubwa wa kazi za matengenezo zilizolala, na kukosa imani kutoka kwa watumiaji wa barabara pamoja na wahisani wa sekta ya barabara.

Ili kuwezesha mabadiliko haya yaanze, Serikali ilitunga Sheria ya ushuru wa Barabara (**The Roads Tolls (Amendment) No.2 Act, 1998)** iliyopelekea kuundwa kwa Mfuko wa Barabara na Bodi ya kusimamia Mfuko wa Barabara. Bodi ya Mfuko wa Barabara ni taasisi iliyosimamiwa na Wizara inayoshugulikia masuala ya Barabara.

Mtandao wa Barabara

Barabara zinazohudumiwa na Mfuko wa barabara kwa mujibu wa sheria ni zile tu zinazolizoorogheshwa katika jedwali la sheria (clasified network) ambazo kwa sasa zina urefu wa kilometa 85,526 kama zinavyoonyeshwa hapa chini:

Jedwali Na. 1: Urefu wa Mtandao wa Barabara

Aina	Barabara za lami (km)	Barabara zisizo za lami (km)	Jumla (km)
Barabara Kuu	3 917	6 027	9 944
Barabara za Mikoa	327	18 629	18 956
Barabara za Wilaya	0	29 537	29 537
Barabara za Mjazio	**0**	21 192	21192
Barabara za Mijini	790	5 107	5 897
JUMLA	5 034	80 492	85 526

Thamani ya mtandao huu wa barabara unakadiriwa kuwa **Tshs. bilioni 3,120** sawa na **US $ bilioni 2.6**.

Jedwali Na. 2: Kulinganisha Takwimu (2003)

	Idadi ya watu	Urefu wa barabara	Eneo	'GDP'	Mapato ya Mfuko	Thamani ya barabara
	milioni	km 000	km² 000	$ bilioni	$ milioni	$ bilioni
Ghana	21	49	238	6.2	75	4.6
Malawi	12	16	118	1.9	15	1.5
Tanzania	38	85	945	17.5	182	2.6

Hapa tunaona thamani ya barabara ni sehemu kubwa ya mali ya nchi ambapo kwa Ghana na Malawi thamani hiyo inakaribiana na GDP. Ni muhimu kutenga fedha za kutosha pamoja na kuimarisha utendaji ili kutunza barabara zetu katika hali endelevu kwa kuwa zina thamani kubwa.

2.0 BODI YA MFUKO WA BARABARA

Dira (Vision) na Maarubu (Mission) ya Bodi

Dira ya Bodi (Vision)

Dira ya Bodi ya Mfuko wa Barabara ni kuwa taasisi ya mfano barani Afrika katika kugharamia matengenezo ya barabara.

Maarubu ya Bodi (Mission)

Maarubu ya Bodi ya Mfuko wa Barabara ni kutoa fedha za kutosha na kwa mtiririko thabiti kwa ajili mya matengenezo endelevu ya barabara na kufuatilia matumizi yake.

Malengo ya Bodi

Malengo ya Bodi ni haya yafuatayo:

(1) Kutoa fedha za kutosha,
(2) Kuhakikisha upelekaji fedha kwa watumiaji na kwa wakati.
(3) Kuhakikisha kuwa fedha zinatumika vizuri ili watumiaji barabara waone thamani ya fedha zao.

Wajumbe wa Bodi

Wafuatao ni wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Barabara:

Jedwali Na. 3: Wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Barabara

S/N	JINA	UTEUZI	ASASI ANAYOIWAKILISHA
1.	Bw. Philip Alfred Magani	Mwenyekiti	Sekta Binafsi
2.	Inj. O. Chambo	Mjumbe	Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu

S/N	JINA	UTEUZI	ASASI ANAYOIWAKILISHA
3.	Bibi M. Tarishi	Mjumbe	Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
4.	Bw. G. Mgonja	Mjumbe	Katibu Mkuu Wizara ya Fedha
5.	Inj. P.A. L. Mfugale	Mjumbe	Mkurugenzi wa Barabara Vijijini, Wizara ya Miundombinu
6.	Bw. M.A. Akunaay	Mjumbe	Chama cha Waendeshaji Utalii
7.	Bw. Ally Hemed Saidi	Mjumbe	Chama cha Wasafirishaji Tanzania
8.	Inj. Aloys J. Mwamanga	Mjumbe	Chama cha Wafanya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania
9.	Nafasi Wazi	Mjumbe	Mjumbe toka sekta binafsi

Bodi ina Sekretariat inayofanya kazi za Bodi za siku hadi siku. na ina wafanyakazi 11 kama ifuatavyo:



3.0 MAJUKUMU YA BODI YA MFUKO WA BARABARA

Majukumu ya Bodi kama yalivyoainishwa katika Sheria Na. 2 ya mwaka 1998, kuhusiana na Mfuko miongoni mwa majukumu mengine ni:

- Kumshauri Waziri kuhusu vyanzo vipya vya ushuru wa barabara, marekebisho ya viwango vilivyopo vya ushuru na kuhusu kanuni za ukusanyaji wa ushuru wa barabara kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwepo kwa mtiririko wa kutosha na wa uhakika wa fedha kwa ajili ya shughuli za barabara,

- Kuhakikisha kunakuwepo na ukusanyaji mzuri na upelekaji wa makusanyo ya ushuru wa barabara kwenye Akaunti ya Mfuko;

- Kutoa fedha kutoka kwenye Mfuko kupeleka TANROADS (wakala wa Barabara ya Taifa Tanzania), Serikali za mitaa na wakala nyingine za barabara;

- Kuhakikisha kuwa shughuli za TANROADS, Serikali za Mitaa na Wakala nyingine za barabara na Mfuko zina ufanisi mzuri wa kimahesabu na kiufundi;

- Kufuatilia matumizi ya fedha zilizopelekwa TANROADS, Serikali za Mitaa na wakala nyingine za barabara kwa madhumuni ya malengo ya Mfuko;

- Kutoa mapendekezo mengine yoyote kwa waziri wa Barabara itakayoonekana ni muhimu ili kuiwezesha Bodi kutimiza madhumuni yake,

Aidha, Sheria Na. 2 ya Ushuru wa Barabara (marekebisho) ya mwaka 1998 inaitaka Bodi ya Mfuko wa Barabara kuingia mikataba ya utendaji na Mtendaji Mkuu wa TANROADS au wakala nyingine inayopewa fedha na Mfuko. Bodi pia inatakiwa kuwasilisha taarifa ya mwaka kwa Waziri mwenye dhamana ya barabara katika kipindi cha miezi mitatu, baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha kulingana na shughuli zake na za asasi zilizopewa fedha.

4.0 VYANZO VYA MAPATO

Vyanzo vya mapato kwa mujibu wa sheria ni:
1. Tozo katika petroli na dizeli (Fuel Levy)
2. Ushuru wa magari ya kigeni mipakani (Transit Fees)
3. Faini ya magari yaliyozidisha uzito (Overloading Fees).

Pamoja na chanzo kingine chochote katika kiwango au viwango vitakavyoamuliwa na Bunge mara kwa mara Aidha tozo katika mafuta ndio chanzo kikuu cha mapato kwa sasa. Kwa vile hivi sasa bei ya mafuta katika soko la dunia inapanda mara kwa mara ni muhimu kwa mfuko kupunguza utegemezi huu kwa siku za usoni.

Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Barabara
Kufuatana na Sheria hii Mfuko wa barabara umeanzishwa kwa masharti yafuatayo:

(1) Fedha zote zinazokusanywa kama ushuru wa barabara zitawekwa katika akaunti ya Mfuko huu.

(2) Angalau asilimia **isiyopungua tisini** ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa utunzaji na matengenezo ya dharura ya barabara zilizoainishwa pamoja na gharama za kiutawala zinazohusiana na shughuli hizo katika Tanzania Bara kulingana na mipango ya utendaji iliyoidhinishwa ambayo imepangwa na:

(a) TANROADS kwa upande wa barabara kuu na barabara za mikoa; na
(b) Mamlaka za Halmashauri kwa upande wa barabara za wilaya na miji, kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

(3) Asilimia **isiyozidi kumi** ya fedha iliyowekwa katika Mfuko itatumika kwa uendelezaji barabara pamoja na gharama za kiutawala katika Tanzania Bara kwa kufuata mipango na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

5.0 Mgao wa Fedha za Mfuko

Mfuko wa Barabara unagawiwa kwa taasisi za utekelezaji kama ifuatavyo:



Utaratibu huu uliwekwa kufuatia tamko la Serikali Bungeni kutokana na mapendekezo ya utafiti uliofanywa.

6.0 Utaratibu wa kugawa Fedha za Mfuko

Utaratibu wa kugawa fedha huanzia pale Bodi inapopata kutoka Wiza ya Fedha na Uchumi kiwango cha fedha zinazotarajiwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha husika (budget cealing) na kisha Bodi kuwapatia waatekelezaji viwango vyao vya bajeti kulingana na fomula ya ugawaji fedha. Taasisi za utekelezaji zinazoruhusiwa kisheria kupata fedha za mfuko hutayarisha bajeti na programu zao za kazi kwa kushirikisha kuzingatia maoni ya bodi za barabara za mikoa na baraza la kanseli ya Halmashauri na kisha kuridhiwa na Asasi zinazowasimamia. Bajeti na programu hizi huwasilishwa na kupitiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kupata idhni ya kuwasilishwa kwa Mawaziri wenye dhamana na barabara kuu na za mikoa na zile zilizo chini ya halmashauri ili awasilishe Bungeni. Baada ya kupitishwa na Bunge Bodi hutayarisha Mikataba ya Utendaji kazi ikihusisha bajeti na programu za kazi kama zilivyopitishwa na Bunge. Baada ya hatua hii bajeti na programu hizo haziwezi kubadilishwa tena na fedha hupelekwa baada ya kusaini mikataba hiyo. Aidha ukaguzi wa matumizi huangalia zaidi jinsi ambavyo Watekelezaji wanafuata Mikata ya Utendaaji.

Mikataba ya Utendaji ni nyenzo muhimu ya kuhakikisha kwamba fedha za Mfuko zinatumika kama zilivyokubaliwa kati ya Bodi na Watekelezaji. Pale inapobainika kwamba fedha zimetumika kinyume na makubaliano Bodi husimamisha kutoa fedha mpaka hapo fedha hizo zinaporudishwa. Mkatataba hii hujumuisha masuala yafuatayo:

(a) Ufafanuzi wa maneno mbalimbali yanayohusiana na matengenezo na ukarabati wa barabara. Katika kipengele hiki, maneno yafuatayo yame fafanuliwa:

Matengenezo ya mara kwa mara (routine maintenance) ni yale yanayofanyika mara kwa mara yakihusisha kazi za kufyeka nyasi kandoni mwa barabara, kusafisha mifereji, kusafisha makalavati na madaraja, kurekebisha alama za barabarani, kuziba mashimo, kuziba nyufa kwenye lami, kupaka rangi kwenye barabara za lami na kuchonga barabara zisizo za lami.

Matengenezo ya muda maalum (periodic maintenance) ni yale yanayofanyika baada ya miaka kadhaa yakihusisha kazi za kurudishia upya tabaka la lami (miaka 7 mpaka 14) au changarawe (miaka 3 mpaka 5).

Ukarabati (rehabilitation) uhesabika kama kazi za maendeleo zikihusisha ujenzi upya wa barabara baada ya kuachwa bila matengenezo ya mara kwa mara na ya muda maalumu kiasi cha kuharibika kabisa. Kwa kawaida gaharama zake ni hadi mara 3 hadi 4 ya gharama za matengenezo ya kawaida na muda maalumu.

(b) Masuala ya kifedha yakielezea kiasi cha fedha zitakazo tolewana matumizi pamoja na masharti yake.

(c) Masuala ya kisera yatakavyoshughulikiwa ikiwa ni pamoja na matumizi ya nguvu kazi, VVU/Ukimwi, uwiano wa jinsia katika ajira , kuajiri wakandarasi wazalendo, utunzaji wa mazingira nk.

(d) Utendaji na ubora wa kazi

(e) Tarehe za kuwasilisha taarifa za utendaji za robo mwaka

(f) Viashiria vya utendaji kazi

MAHITAJI YA FEDHA ZA MATENGENEZO

Kwa mujibu wa makisio yaliyofanyika mwaka 2007, mahitaji ya fedha za matengenezo ya barabara zilizo chini ya Taasisi za Utekelezaji ni kama ifuatavyo:

ROAD NETWORK MAINTENANCE NEEDS FOR FIVE YEARS (TShs. billion)						
1	TRUNK AND REGIONAL ROADS					
S/N	ACTIVITY	FY 2007/08	FY 2008/09	FY 2009/10	FY 2010/11	FY 2011/12
1.1	Routine Maintenance	28.865	29.405	29.946	30.486	31.027
1.2	Periodic Maintenance	108.430	108.430	108.430	108.430	108.430
1.3	Bridge Maintenance	6.865	6.892	6.919	6.946	6.973
1.4	Emergency Repairs	2.887	2.941	2.995	3.049	3.103
1.5	Spot Maintenance	2.616	2.355	2.093	1.831	1.57
1.6	Administration and Supervision	8.823	8.860	8.897	8.935	8.972
1.7	Non Works Activities	1.765	1.772	1.779	1.787	1.794

	SUBTOTAL TShs	**160.251**	**160.655**	**161.059**	**161.464**	**161.869**
	US$ = TShs	1318.200	1336.665	1355.368	1374.343	1393.584
	SUBTOTAL US$	121.568	120.191	118.830	117.484	116.153
2	**DISTRICT, FEEDER AND URBAN ROADS**					
2.1	Routine Maintenance	15.105	15.261	15.573	16.158	16.938
2.1	Periodic Maintenance	38.921	38.921	38.921	38.921	43.001
2.3	Bridge Maintenance	1.450	1.450	1.500	1.500	1.550
2.4	Emergency Repairs	1.000	1.000	1.000	1.000	1.000
2.5	Spot Maintenance[1)]	4.000	8.000	11.500	12.000	11.565
2.6	Administration and Supervision	5.648	5.630	5.699	5.758	6.249
2.7	Non Works Activities	0.000	0.000	0.000	0.000	0.000
	SUBTOTAL in bio TShs.	**66.124**	**70.262**	**74.193**	**75.337**	**80.303**
	SUBTOTAL in mio USD	**50.162**	**52.565**	**54.740**	**54.817**	**57.623**
3	**TOTAL (All roads) in TShs.**	**226.375**	**230.917**	**235.252**	**236.801**	**242.172**
	TOTAL (All roads) in US$ million	171.730	172.756	173.570	172.301	173.776
[1)] Envisaged to be financed by Development Partners						

Kulingana na mahitataji hayo ni wazi mahitaji ya Wakala wa Barabara ni karibu mara mbili na nusu ya mahitaji ya Halmashauri. Hii inatokana na ikweli kwamba TANROADS ina barabara nyingi za lami na changarawe ukilinganisha na zile zlilizo chini ya Halmashairi ambazo huhitaji fehda nyingi kuzihudumia. Aidha barabara nyingi zilizo katika Halmashauri ni mbovu na hivyo huhitaji fedha za maendeleo zaidi ili ziweze kuhitaji fedha za matengenezo. Aidha bajeti ya TAMISEMI au Halmashauri kwa mwaka huu wa fedha (ukiondoa mahitaji ya fedha za maendeleo) inakidhi mahitaji ya matengenezo ya kawaida na yale ya maalum. kwa asilimia 100.

Fedha Zilizokusanywa Kutoka Vyanzo Vya Mfuko

Jedwali Na. 4: Makusanyo ya miaka saba iliyopita

	2000/01 Tshs. (Bilioni)	2001/02 Tshs. (Bilioni)	2002/03 Tshs. (Bilioni)	2003/04 Tshs. (Bilioni)	2004/05 Tshs. (Bilioni)	2005/06 Tshs. (Bilioni)	2006/07 Tshs. (Bilioni)
Tozo ya Mafuta	44.940	50.131	55.867	64.113	67.845	69.524	94.850
Malipo ya magari ya kigeni yapitayo mpakani	1.150	1.302	1.516	1.406	1.658	1.951	2.885
Malipo ya magari yanayozidisha uzito	1.162	1.356	1.856	1.635	3.525	1.606	3.480
Leseni za magari makubwa	-	.092	.151	.188	.176	0	0
Jumla	**47.252**	**52.881**	**59.390**	**67.342**	**73.204**	**73.081**	**101.215**

Migao ya fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2000/01 hadi 2006/07 ilikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 5: Migao ya Fedha za Mfuko kwa miaka saba iliyopita

Mwaka wa Fedha	TANROADS Tshs. (Bilioni)	Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI Tshs. (Bilioni)	Wizara ya Miundombinu Tshs. (Bilioni)	Bodi ya Mfuko wa Barabara Tshs. (Bilioni)	Jumla Tshs. (Bilioni)
2000/01	25.632	10.846	2.927	0.624	40.030
2001/02	31.390	15.240	3.488	0.620	50.738
2002/03	41.648	19.302	4.450	0.674	66.074
2003/04	40.206	19.146	4.467	0.691	64.510
2004/05	45.788	21.804	5.088	0.734	73.414
2005/06	46.738	22.256	5.193	0.862	75.049
2006/07	53.322	25.442	5.925	1.054	85.743
TOTAL	**284.724**	**134.036**	**31.538**	**5.259**	**455.558**

NB: Tofauti kati ya makusanyo na migao ni kati ya fedha zilizokusanywa mwaka wa fedha 2006/2007, kupokelewa na kugawiwa katika mwaka wa fedha 2007/2008. Taarifa za mapato na migao kwa mwaka 2007/2008 zitapatikana baada ya ukaguzi wa fedha (financial audit) unaoendelea kukamilika.

Jedwali Na. 6: Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Fedha za ndani

	Tshs. (Bilioni)
Tozo ya Mafuta (Fuel levy)	218.474
Malipo ya magari ya kigeni yapitayo mpakani (Transit Fees)	0.227
Jumla	**218.701**

Aidha Bodi ya Mfuko inategemea kupokea fedha za nje **Tsh. 34.055** billioni toka Serikali ya **Denmark** ikiwa ni msaada kwa ajili ya bajeti ya matengenezo ya barabara (budget support).

Jedwali Na. 7: Migao kwa Asasi za Utekelezaji mwaka wa fedha 2008/2009

Mapendekezo ya Migao kwa Asasi za utekelezaji mwaka wa fedha 2008/2009 kwa bajeti ya tozo ya mafuta pekee

Asasi	**Bajeti i**
Toa Fedha za Uendeshaji wa Mfuko	218,474,400,000
Less Road fund administration (0.8%)	-1,857,100,000
	216,617,300,000
Wakala wa Barabara (TANROADS)	136,468,899,000
Wizara ya Miundombinu (MOID)	15,163,211,000

TAMISEMI	64,985,190,000
Mfuko wa Barabara	1,857,100,000
Jumla	**218,474,400,000**

Fedha za msaada toka Denmark zina masharti yake ya mgao na matumizi kama ifitavyo:

- Local Roads District Roads Development: **Tsh. 1.805 Billion**

- National Roads strengthening and Regional Roads backlog Maintenance **Tsh. 32.25** billion.

Mchanganuo wa mikoa, Halmashauri na barabara zitakazofaidika na msaada huu umo katika bajeti za taasisi za utekelezaji husika.

UFUATILIAJI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA MFUKO

Bodi hufuatilia matumizi ya fedha za mfuko kwa njia tatu ambazo ni:

(i) Taasisi zinazopokea fedha za mfuko hutakiwa kuwasilisha ripoti za robo mwaka kuonyesha matumizi ya fedha dhidi ya kazi zilizofanyika.

(ii) Wajumbe wa Bodi na Sekretariat hutembelea taasisi za barabara. Bodi imetembelea mikoa yote tangu ianze.

(iii) Kunafanyika ukaguzi wa kimahesabu na ya kiufundi kubaini ikiwa kazi za barabara zina thamani ya fedha (value for money) na manufaa kiuchumi na kijamii (socio-economic benefits) kwa wanachi waishio sehemu zinakofanyika kazi hizo.

ROADS FUND BOARD

Telephone: +255 22 2125916-7
Fax No. +255 22 2124339
E-mail: roadfund@raha.com

2nd Floor

TETEX BUILDING

Pamba Road

P.O. Box 12497
DAR ES SALAAM

TANZANIA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BARABARA ZITAKAZOTENGENEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2008/2009

Bodi ya Mfuko wa Barabara inatangaza kwamba barabara, madaraja na kazi za barabara zifuatazo zitatengenezwa / zitafanyika katika mwaka wa fedha 2008/2009 kama zilivyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania katika Bajeti za Wizara za Maendeleo ya Miundombinu na TAMISEMI.

Barabara, madaraja na kazi za barabara ni zile zitakazofanyika kwa kutumia fedha za mfuko pekee au Mfuko wa Barabara kuchangia utekelezaji wake na haijumuishi kazi zitakazotekelezwa kutokana na fedha toka Mfuko Mkuu wa Serikali na Wafadhili mbalimbali. Aidha orodha hii haijumuishi kazi ndogo ndogo za matengenezo ya kawaida “routine / recurrent maintenance”; yaani zile zinazohusisha kuziba mashimo barabarani, kufyeka nyasi kusafisha / kuzibua mifereji, kusawazisha barabara (grading) n.k. Hizi zitafanyika kwa barabara zote zilizo katika hali nzuri na za wastani ambazo nazo zimepangiwa fedha za kutosha kutoka Mfuko wa Barabara. Orodha ya kazi ndogo ndogo inapatikana katika Ofisi za Wahandisi wa Mikoa TANROADS na za Halmashauri husika.

Bodi inapenda kufahamisha umma pia kwamba itafanya ukaguzi wa masuala ya fedha (Financial Audit) na ule wa kiufundi (Technical Audit) kwa kutumia wataalamu mahususi ili kubaini endapo kazi hizo zina thamani ya fedha (Value for Money) na zimeleta manufaa ya kiuchumi na kijamii (socio-economic impact) kwa Wananchi wanaoishi katika maeneo hayo na jamii kwa ujumla. Msisitizo uliopo ni kwamba kwa kiasi kikubwa kazi zote zitakazofanyika katika barabara hizi lazima zifanywe kwa kutumia raslimali watu inayopatikana katika maeneo husika ili kuongeza kipato na kupunguza umaskini katika maeneo hayo. Ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha 2008/2009 tangazo kama hili litatolewa kuelezea maendeleo ya utekelezaji wa kazi hizo.

Wananchi kwa kupitia Halmashauri za Wilaya na Bodi za Barabara za Mikoa wanaombwa kufuatilia utekelezaji wa kazi hizi katika Mikoa yao ili kuhakikisha thamani bora ya huduma hizi inapatikana kabla ya mwisho wa Mwaka wa Fedha kuisha.

J.O. Haule
Katibu Bodi ya Mfuko wa Barabara